**DCB Commercial Bank Plc**

## TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA NNE WA WANAHISA

Taarifa inatolewa kwamba, Mkutano Mkuu wa Ishirini na Nne wa Mwaka wa DCB Commercial Bank Plc, utafanyika siku ya Ijumaa tarehe 26 Juni 2026 kwa njia ya mtandao, kuanzia saa nne kamili (4:00) asubuhi.

**Agenda**

1. Kufungua Mkutano Mkuu Wa Mwaka
2. Kuridhia agenda ya Mkutano Mkuu wa Ishirini na Nne wa Mwaka
3. Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa 23 wa Mwaka uliofanyika tarehe 19 Julai 2025
4. Kupokea na kuridhia utekelezaji wa yatokanayo na Mkutano Mkuu wa 23 wa Mwaka
5. Kupokea na kuridhia
   - 5.1 Taarifa ya wakurugenzi ya mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba, 2025
   - 5.2 Taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba, 2025
   - 5.3 Taarifa ya mkaguzi huru ya hesabu zilizokaguliwa za mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba, 2025
6. Kupokea taarifa ya kuisha kwa muda wa wajumbe wa Bodi ya wakurugenzi
7. Uchaguzi wa wajumbe wa Bodi ya wakurugenzi
8. Kupokea na Kuidhinisha uteuzi wa Mkaguzi Huru wa hesabu kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Disemba 2026
9. Kupokea na kuridhia pendekezo la malipo ya ada kwa wajumbe wa bodi
10. Kupanga tarehe ya Mkutano Mkuu wa 25
11. Mengineyo
12. Kufunga mkutano

**MAELEZO**

1. Wanahisa wanaotarajia kuhudhuria mkutano mkuu wanatakiwa wawe na CDS namba ambazo zinapatikana kwenye risiti ya uwekezaji wa hisa (depository receipt) au taarifa ya akaunti (CSDR account statement).
2. Wanahisa ambao hawataweza kuhudhuria Mkutano wanaruhusiwa kuchagua wawakilishi watakaohudhuria na kupiga kura kwa niaba yao kwa kufuata/kuzingatia sheria na Katiba ya Kampuni. Fomu ya uwakilishi (Proxy Form) lazima ijazwe na kuwasilishwa kwenye ofisi ya Katibu wa Benki iliyopo Makao Makuu ya Benki ya DCB au kwa njia ya mtandao kupitia barua pepe shareholder@dcb.co.tz au matawini kabla ya saa 4 asubuhi siku ya Alhamisi tarehe 25 Juni 2026
3. Nakala za taarifa ya mwaka na fomu za mwakilishi (proxy forms) zitapatikana matawini na kwenye tovuti ya benki (www.dcb.co.tz).
4. Kufungwa kwa orodha (Register) ya wanahisa tarehe 22 Juni 2026
5. Mapendekezo ya wanahisa yawasilishwe kwenye ofisi za makao makuu zilizoko jengo la DCB Magomeni Mwembechai au kwa barua pepe kabla ya saa 8.00 mchana siku ya Jumatano tarehe 24 Juni 2026.

**KWA IDHINI YA BODI,**

**Regina Mduma**
**Katibu wa Kampuni**
**2 Juni 2026**